TANGAZO LA SERIKALI Na. 224 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MMOVO YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Mmovo ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Kuandaa na kuhifadhi Mipangokina

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala.

———

JEDWALI

———

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M1 yenye majira – nukta 536486MS, 8821942KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa $76^0$ 10'05'' kwa umbali wa kilomita 1.07 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M2 yenye majira - nukta 535456MS, 8821683KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $18^0$ 50'25'' kwa umbali wa kilomita 1.85 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M3 yenye majira - nukta 536051MS, 8819937KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $63^0$ 14'35'' kwa umbali wa kilomita 2.195 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M4 yenye majira - nukta 538012MS, 8820926KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa kufuata barabara ya Kitangari – Mtopwa hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*